# MAOMBI

## Ya Kujikuza kiroho

TOLEO LA 7



**BY DENIS & DEVIS JULIUS**

**MAOMBI MAALUMU YA KUJIKUZA KIROHO.**

**~Toleo la 7**

**UTANGULIZI:**

Huu ni mwendelezo wa maombi maalumu ya kujikuza kiroho. Kama watoto wa Mungu lazima tufahamu tusipokuwa na bidii katika kuomba, maisha yetu ya rohoni yatakuwa ni mazito kuendelea. Yapo mambo ambayo Mungu atatujalia pasipo sisi kuomba, lakini pia yapo mambo ambayo kamwe hatuwezi kupokea kama sisi hatutaomba, mojawapo ikiwa hili la kukua kiroho, Maombi sio tendo la kujisikia, bali ni tendo endelevu. Kama mwaminio kila siku omba, kama vile ulavyo kila siku, hususani katika eneo hili la ukuaji kiroho.(1Petro 2:2, 2Petro 3:17-18).

Pia kumbuka maombi pamoja na Neno la Mungu ndani yako, Ndio lishe kamili ya kiroho, Hivyo tembelea website yetu hii www.wingulamashahidi.org. Ukutane na mafundisho mengi, zaidi ya 4,000 ikiwemo na majibu ya maswali mengi ya biblia, yatakayokusaidia kuelewa biblia kwa upana wake.

Mwongozo huu ni wa SAA SITA (6) kwa wiki. Ikiwa hujapata mwendelezo wa nyuma, basi wasiliana nasi kwa namba unazoziona chini ya makala hii. Tutatoa na dakika za kuombea kila kipengele, mpaka kile cha mwisho kitakapomalizika. Katika maombi haya pendelea kujiwekea ratiba yako maalumu, ya kuomba, hiyo itakusaidia kuwa na nidhamu ya kiroho. Lakini usiombe tu ilimradi leo umejisikia, chukulia kwa umakini maisha yako ya rohoni.

Karibu sasa katika mwongozo wetu..

~Mwl Denis & Devis Julius

# <u>MBEGU NJEMA MOYONI MWAKO</u>

**<u>(Mathayo 13:3-9)</u>**

Bwana Yesu alisema maneno haya.

*Mathayo 13:3  Akawaambia mambo mengi kwa mifano, akisema, Tazama, mpanzi alitoka kwenda kupanda. 4  Hata alipokuwa akipanda, mbegu nyingine zilianguka karibu na njia, ndege wakaja wakazila; 5  nyingine zikaanguka penye miamba, pasipokuwa na udongo mwingi; mara zikaota, kwa udongo kukosa kina; 6  na jua lilipozuka ziliungua; na kwa kuwa hazina mizizi zikanyauka. 7  Nyingine zikaanguka penye miiba; ile miiba ikamea, ikazisonga; 8  nyingine zikaanguka penye udongo mzuri, zikazaa, moja mia, moja sitini, moja thelathini. 9  Mwenye masikio na asikie.*

Ukichunguka mkulimu huyu, mbegu alizokuwa anazipanda sio mbegu za kuchimba chini kama vile mtu apandavyo mahindi, hapana, bali ni mbegu za “kurusha” kama vile upandavyo mchicha,. Na lengo la mkulima ni zifikie kwenye udongo alioundaa zikue zizae. Lakini kwa kawaida si zote huwa zina nguvu ya kufika pale, zipo ambazo zitaangukia sehemu nyingine, kwasababu ni nyingi zinazorushwa.

Ndio hapo, anasema nyingi zikaangukia palepale njiani, nyingine, kwenye miamba, nyingi kwenye miiba, na nyingine kwenye udongo mzuri,.

Kufananisha na maisha ya kiroho ya mwaminio. Hupitia sehemu hizi kuu 4, ili afikie hatua ya kuona uhai wa Neno la Mungu ndani yake, au maisha yake ya rohoni kuwa na matunda.

Hivyo katika mwongozo huu tutaombea hatua zote nne.

## <u>NJIANI: (Dk 90)</u>

Yesu alitoa tafsiri yake akasema..

*Mathayo 13:19  Kila mtu alisikiapo neno la ufalme asielewe nalo, huja yule mwovu, akalinyakua lililopandwa moyoni mwake. Huyo ndiye aliyepandwa karibu na njia.*

Unaweza ukawa msikiaji tu, sikuzote, lakini ufahamu wako ukawa umefungwa hauelewi ni nini Bwana anataka ukifahamu. Na hiyo ikakupelekea  kuwa vilevile rohoni ijapokuwa ameshasikia sana mahubiri, ameshasoma sana Neno. Lakini shetani anafanya kazi ya kuliondoa Neno la Mungu ndani yako.

**Maombi**:

- ✓ Omba Bwana akuongezee uelewa wa rohoni, ili usiwe mzito kumwelewa Mungu pindi akufundishapo.

*Luka 24:45 Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko*

- ✓ Omba Bwana akuongezee uwezo wa kukumbuka maagizo yake yote. Ili usiwe msikaji msahaulifu.

*Yohana 14:26 Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia.*

- ✓ Omba Bwana aweke umuhimu wa kulitafakari Neno lake, kwa muda mrefu ndani yako.
- ✓ Omba Bwana akupe uwezo wa kuletendea kazi Neno lake pindi usomapo au ufundishwapo.
- ✓ Omba asafishe vyumba vya moyo wako, ili Neno lipate nafasi ya kukaa na kutafakariwa. Auie kiu ya mambo mengine kama Tv, michezo, n.k
- ✓ Omba Mungu akulinde ufahamu wako, ili ibilisi asipate upenyo wa kukuingia na kukupotosha, au kulinyakua Neno la Mungu lililoingia moyoni mwako.

## PENYE MIAMBA: (Dk 90)

*Mathayo 13:20 Naye aliyepandwa penye miamba, huyo ndiye alisikiaye lile neno, akalipokea mara kwa furaha; 21 lakini hana mizizi ndani yake, bali hudumu kwa muda; ikitukia dhiki au udhia kwa ajili ya lile neno, mara huchukizwa.*

Shetani akishaona unalitunza Neno la Mungu moyoni mwako, ataamsha na vita vingine, vya kukuhangaisha kwa majaribu mbalimbali, lengo lake ni kuhakikisha wewe haufikii ukomavu wa kiroho.

**Hivyo omba:**

- ✓ Bwana akuepushe na majaribu yote ya Yule mwovu.

*Luka 22:40 Alipofika mahali pale aliwaambia, Ombeni kwamba msiingie majaribuni.*

- ✓ Bwana akupe uthabiti wa moyo: Ujikutapo katika majaribu yoyote (ikiwa ni lazima kuyapitia), basi uweze kuyashinda. Usiwe kama unyasi unaotikiswa na upepo.

- ✓ Akuongezee Ujasiri: Tukikosa ujasiri katika changamoto mbalimbali tunazopitia kwa ajili ya Kristo, ni rahisi kupoa. Hivyo eneo hili ni muhimu pia kuombea kwenye maisha yako, Bwana aondoe woga wote.
- ✓ Aongeze furaha na amani moyoni mwako katika nyakati zote.

*Mathayo 5:11 Heri ninyi watakapowashutumu na kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili yangu.12 Furahini, na kushangilia; kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu.*

## **PENYE MIIBA: (Dk 90)**

*Mathayo 13:22 Naye aliyepandwa penye miiba, huyo ndiye alisikiaye lile neno; na shughuli za dunia, na udanganyifu wa mali hulisonga lile neno; likawa halizai*

Pia Luka inasema..

*Luka 8:14 Na zilizoanguka penye miiba ni wale waliosikia, na katika kuenenda kwao husongwa na shughuli na mali, na anasa za maisha haya, wasiivishe lo lote.*

Adui akiona umelitunza Neno la Mungu, umestahimili dhiki kwa ajili ya Kristo, sasa anakuja kwa njia ya undanganyifu wa mambo ya kidunia. Ndio hapo, anakuletea anasa, shughuli nyingi, utafutaji mali uliopitiliza ili tu upoteze muda usilizalie matunda Neno lile.

**Omba**

- ✓ Bwana akupe muda mwingi wa kuwa karibu na yeye. Muda ni muhimu kujijenga kiroho.
- ✓ Akupe kuviona na kujitenga na vishawishi vyote vya kidunia, vinavyokuweka mbali na kusudi la Mungu. Kampani za watu wabaya, shughuli zilizovuka mipaka n.k.
- ✓ Aiue tamaa ya mambo mbalimbali, yasiyokunufaisha roho yako.
- ✓ Akupe kuridhika na vile alivyokujalia

## **PENYE UDONGO MZURI: (Dk 90)**

*Luka 8:15 Na zile penye udongo mzuri, ndio wale ambao kwa unyofu na wema wa mioyo yao hulisikia neno, na kulishika; kisha huzaa matunda kwa kuvumilia.*

Hatua hii ndio ya mwisho, ambayo mkristo ukiweza ifikia basi, unakuwa mtu mwingine rohoni. Nayo ni udongo mzuri. Lakini tunaona,mbegu zake zilizaa kwa kuvumilia, na unyofu wa moyo.

**Omba**

- ✓ Bwana akupe unyofu wa moyo: Si kigeugeu, au mwenye nia mbili.
- ✓ Bwana akupe uvumilivu katika imani: Ukikosa uvumilivu hatua zote tatu huwezi kuzivuka, omba sana Bwana akujengee tunda hili rohoni.
- ✓ Bwana akupe kulipenda Neno lake: Ukilipenda Neno lake utakuwa radhi, kukabiliana na vishindo vyote vya Mwovu.

Hivyo ukiweza kuimarisha kwenye maeneo hayo manne, basi pale Bwana anataka ufikie bila shaka utafikia, na utaona matunda mengi sana katika ukristo wako.

Bwana akubariki sana.

Mwendelezo mpya unakuja...

Kwa ushauri/ Msaada/ Maombezi wasiliana nasi kwa mawasilino haya;

Na, Mwl Denis & Devis Julius
Nuru_ya_ Upendo
Website: www.wingulamashahidi.org
Email: info@wingulamashahidi.org
+255693036618/ +255789001312